Teacher.co.ke

# SHULE YA UPILI YA MARANDA

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

MTIHANI WA MWIGO 2021

102/3 KISWAHILI (FASIHI) Karatasi ya 3

Disemba 2021 – Saa: 2½

Jina : ………………………………………….. Nambari yaUsajili: ………….

Mkondo: ………… Sahihi ya mtahiniwa: ……….. Tarehe: ……./12/2021.

**Maagizo**

a) *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
c) *Swali la kwanza ni la* ***lazima****.*
d) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Ushairi, hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*
e) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
f) *Karatasi hii ina kurasa* ***14****. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*
g) *Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

## KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Teacher.co.ke



## SEHEMU A: TAMTHILIA

**Pauline Kea:** *Kigogo*

**1. Lazima**

"Nimekuja kuwakomboa. Si kuwaumbua. Hali hii si hali. Kuna leo na kesho. Na kesho hujengwa na leo."

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

b) Bainisha mitindo **minne** ya lugha inayojitokeza katika dondoo. (alama 4)

c) Eleza michango **kumi na miwili** ya msemewa katika kudidimiza kauli iliyopigwa mstari kwa kurejelea tamthilia *Kigogo*. (alama 12)

## SEHEMU B: RIWAYA

**Assumpta K. Matei**: *Chozi la Heri*

*Jibu swali 2 au 3*

2. "Unajua kwamba mimi sikuumbiwa ujalaana, walimwengu ndio walionifinyanga upya, wakanipa moyo wa ujabari."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Changanua mtindo katika dondoo. (alama 4)

c) Kwa kurejelea wahusika wowote **kumi na wawili** katika riwaya *Chozi la Heri*, thibitisha ukweli wa kauli iliyopigwa mstari. (alama 12)

3. a) Kwa kutolea mifano katika riwaya *Chozi la Heri*, jadili jinsi mwandishi alivyotumia migogoro ya kisiasa kufanikisha ploti. (alama 10)

b) Kwa kurejelea barua ya kumstaafisha Lunga, jadili jinsi mwandishi alivyofanikisha maudhui katika riwaya. (alama 10)

## SEHEMU C: USHAIRI

*Jibu swali 4 au 5*

4. *Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata*

Jogoo anapowika, ana jambo atangaza
Atangaza kuamka, limeshatanduka giza,
Giza limeshaondoka, uache kujidumaza,
Mwanamke amka!

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Teacher.co.ke

Jogoo anapowika, mwanamke amjuza
Amjuza kuamka, amulikwe na mwangaza,
Mwangaza umeshafika, aache kujilegeza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke ahimiza,
Ahimiza kutimka, mbio ili kujikuza,
Kujikuza si dhihaka, elimu kuitukuza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke amkuza,
Amkuza kuzizika, tamaduni za kuviza,
Kuziviza kwa haraka, mila zinazopumbaza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke atukuza,,
Atukuza amefika, kupokea yake tuza,
Tuza ya kurevuka, muamko kutangaza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke akataza,
Akataza kutotaka, minyanyaso ya kuliza,
Kuliza na kuudhika, hakiye kugandamiza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke amwongoza,
Amwongoza umefika, muda wa kuongoza,
Kuongoza kwa hakika, umma pasi kujitweza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke azoweza,
Azoweza kurauka, kwa bidii kujikaza,
Kujikaza na kutoka, jikoni kulomviza,
Mwanamke amka!

a) "Mtunzi wa shairi hili ananuia kumzindua nafsinenewa." Jadili. (alama 7)

b) Ainisha bahari **sita** za shairi hili. (alama 6)

c) Onyesha mbinu **tatu** alizozitumia mshairi kukidhi mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (alama 3)

d) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha tutumbi. (alama 4)

5. *Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata*

Kiza nene kimetanda
Ukungu na umande
Zinashindana
Umweso unamulika
Radi nayo inapiga
Kimya!

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Bundi na milio yao
Ama kweli, kimila si mazuri mambo.
Mebainika usiku, usiku mkuu, wa kiza nene.
Kiza! Kiza! Kiza!
Balaa! Balaa! Balaa!
Beluwa! Beluwa! Beluwa!
Sinyaa! Sinyaa! Sinyaa!

Kabla,
Inajipenyeza kwa umbali
Kwa umbali hakika
Inuka! Zungumza! Wamefika!
Hakika, sina cha kuwaeleza!
Hakika, zaidi ya kuwakemea, kuwakemea, kuwakaripia, kuwafokea,
Hakika, hakuna kutia, hakuna kutoa
Hakika, Hisabati kueleweka hakupo.
Haki, ukiukaji, melandana kama ulimi na mate!

Dovu hili dovu kubwa!
Lima hili, pandikizi
Uzito wa nanga, kukwepa hakukwepeki.
Wanasema faraghani, kwa mihemko!
"Watatu maghulamu,
Zao la ushuhuba, kando na mkataba."
Ingawa, kwangu mimi, maana yaniambaa.

Kabla,
Najua fika kuwa,
Tumbo ndilo kisukumo, chanzo hasa.
Uki ulioacha, ndicho chanzo cha migogoro.
Migogoro isiyo ukomo
Kutokomea tokotoko.
Kwangu mezaa madhara.

Lakini.

Kabla ya Kabla,
Hafifu maninga yanatazama
Mwanga ukinyemelea,
Ishara kuwa,
"Yamekwisha!"
Tetesi zimekuwa feki! Kwa vile,
Nijuavyo,
Hata wawili wetu mabanati,
Hakika,
Ni zao la takrima ya akraba yako mnuna.
Hakika,
Ulikuwa ardhi tambarare.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

a) Kwa kutolea mifano, fafanua masuala makuu **sita** anayoyazungumzia mshairi. (alama 6)

b) Onyesha vipengele vifuatavyo vilivyotumika katika shairi. (alama 6)

i) Aina za taswira

ii) Taashira

iii) Aina za usambamba

c) Huku ukitolea mifano, bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

d) Fafanua toni inayojitokeza katika ubeti wa mwisho. (alama 2)

e) Pambanua muundo wa shairi hili. (alama 4)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

*Jibu swali 6 au 7*

**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda**: *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

**Eunice Kimaliro**: Mtihani wa Maisha

6. a) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia uzungumzinafsi kukuza wahusika katika hadithi *Mtihani wa Maisha*. (alama 8)

**Salma Omar Hamad**: *Shibe Inatumaliza*

b) "Lakini nakwambia tena, kula kunatumaliza."

"Lakini kula kunatumaliza vipi?"

i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 5)

ii) Jadili jinsi mandhari ambamo mazungumzo haya yamejikita yanafanikisha maudhui katika hadithi hii. (alama 7)

**Alifa Chokocho**: *Tulipokutana Tena*

**7.** a) "Kwa nini walinitoa na kunisabilia kuwa mbali na wao? … <u>Nilihisi kwamba waliniuza au walinitupa</u>."

Tumia usimulizi wa msemaji kutathmini ukweli wa kauli iliyopigwa mstari**.** (alama 9)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Teacher.co.ke

**Ali Abdulla Ali**: *Ndoto ya Mashaka*

b) Jadili mbinu-ishi zinazoibuliwa na wahusika mbalimbali katika hadithi hii. (alama 6)

c) Changanua mtindo: (alama 5)

“Siku zilijumuika zikawa majuma, majuma yakaungana na kuunda miezi na miezi ikaunda miaka. Nakumbuka siku moja … siku hiyo hatuna hili wala lile. Tulikuwa ndani tukipiga gumzo. Mimi na Waridi. Si unajua tena mambo ya utoto? Mimi nilikuwa barobaro zima na Waridi, mwanamwari. Ghafla tulisikia teke *puu* … na kilango *ng’waa* … kikasalimu amri!”

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. *Soma utungo ufuatao kisha uutumie kujibu maswali yanayofuata*

Jua limechomoza leo likiwa kali angani
Majira ni ya asubuhi rafiki,
Akilini sijasahau
Aliyonipitishia, akishatindiika,
Aibu ikanitwaa na wahaka kunivaa.

Kadamnasi alifika hadharani kumimina
Cheche moto za matusi ziso mithilika.

Teacher.co.ke

Ila leo nasema kwa alofanya,
Amani nawe na muwe ardhi na mbingu
Pamoja nawe jamaa zako wakuandame
Katika uchochole ulitima wa kimawazo
Mazao yako na yanyaukie kondeni!
Mifugo wako na wafie malishoni!
Uhangaishwe nao mara elfu na elfu!
Ujinga na daima urithishwe kimapokeo.
Utulivu na ukugure daima dawamu!

a) Tambua kipera cha mazungumzo kinachorejelewa. Thibitisha jibu lako kwa mifano **mitatu**. (alama 4)

b) Kwa kutolea ithibati, taja shughuli zozote **mbili** za kiuchumi zinazotekelezwa na jamii inayorejelewa katika kipera hiki. (alama 2)

c) Fafanua umuhimu wa nidaa katika kufanikisha uwasilishaji wa kipera hiki. (alama 3)

d) Onyesha matokeo **matatu** ya kutenda kinyume na matarijio ya jamii inayorejelewa katika kipera hiki. (alama 3)

e) Kwa hoja **nane**, eleza namna shule yako inavyochangia kukuza vipera mbalimbali vya fasihi simulizi. (alama 8)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

……………………………………………………………………………………………………………

………………………………….............

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes